GRACE COMMUNION INTERNATIONAL

"I am in My Father, and you in Me, and I in you" (John 14:20)

**Viongozi na Mungu**

**Viongozi** wa Kanisa huwa wameitwa na Mungu, na kutengwa kwa ajili ya injili, Warumi 1:11; 1 Wakorintho 1:1, wawe watumishi Yohana Mtakatifu 13:4-17, 21:9-12, Matendo ya Mitume 26:16, kwa ajili ya Kanisa lililochaguliwa na Mungu, Wakolosai 1:25.

Kutokana na kuchaguliwa huku, kiongozi wa kanisa anawajibika moja kwa moja kwa Mungu, Yohana Mtakatifu 12:45; 14:10; Matendo ya Mitume 4:19; 5:4; Warumi 14:12, na haya yote yanatendeka ndani ya uwajibikaji wa mtililiko wa utawala wa Kanisa, Matendo ya Mitume 20:28. Viongozi wanamnyenyekea Mungu 2 Wakorintho 5:11, Waefeso 3:14, Matendo ya Mitume 9:31 na kuwa makini kuhusu maisha yao na kanuni za imani za Kanisa 1 Timotheo 4:16; 2 Wakorintho 5:9, ili kutukuza Mungu katika ushirka wao, Yohana Mtakatifu 11:4; 13:31; 14:13.

**Viongozi** wanaongozwa na Roho Mtakatifu, Warumi 8:9, hupendekezwa na kuonyeshwa wakiwa wema na Yesu Kristo, Warumi 16:10; 1 Thesalonike 2:4.
Wanamtukuza Mungu; Matendo ya Mitume 4:24; 13:2; 16:25, 2 Wakorintho 1:3, na inapobidi wanaadaliwa kwenda kivyao Yohana Mtakatifu 6:66-67; 7:5. Pamoja na kwamba wanatambua hakuna wakati wanakuwa peke yao, kwa kuwa Mungu yuko pamoja nao, Yohana Mtakatifu 6:32.

**Yale viongozi wanajua.**

**Viongozi** wanao uelewa kuhusu ufalme wa Mungu, Warumi 14:17 na pia uelewa wa nyakati zilizopo, Warumi 13:11. (Na pia huo muda ni mfupi) 1 Wakorintho 7:29.
Hawaenezi uvumi kuhusu kurejea kwa Kristo 1 Thesalonike 5:1-2

**Viongozi** wanajaribiwa na adui zao, Yohana Mtakatifu 8:6. Na pia wanatakiwa kuwa tayari kuwasamahe  Matendo ya Mitume 7:59-60; 2 Wakorintho 2:1, Uongozi wao unatakiwa kuwa wa karibu na wanao ongozwa, sio wa kupitisha hukumu, Yohana Mtakatifu 5:45; 6:37, 40.

**Viongozi** wanaelewa kuwa Mungu aliwaumba kwa lengo maalum, 2 Wakorintho 5:5, Waefeso 1:4, Waefeso 1:5; Yohana Mtakatifu 12:27, 13:1, 13:3, 18:37.
Wanapenda kutii Mungu kuliko wanadamu, Matendo ya Mitume 4:19; 8:26-27; Warumi 1:5 hata kuhatarisha maisha yao, 1 Wakorintho 15:3, Matendo ya Mitume 7:57-60; Yohana Mtakatifu 19:6.

**Tabia na uwezo wa viongozi.**

**Viongozi** wanatenga muda na kuwa na Mungu pekee, Yohana Mtaakatifu 6:15, 8:1
Wamebatizwa , Matendo ya Mitume 9:18; Warumi 6:4
Wanafuraha Wafilipi 1:4-5, Warumi 5:2-3,
Wanashukurani, Matendo ya Mitume 28:15, Warumi 1:8, 6:17; Waefeso 1:16,
Mara kwa mara wanaomba, Matendo ya Mitume 2:42; 3:1; Waefeso 3:14-21, Warumi 1:9-10,
Wamejazwa neema na nguvu, Matendo ya Mitume 6:8.

**Viongozi** wanatakiwa wawe na uwezo wakufikiria nje ya matarajio ya wengi, Yohana Mtakatifu 6:20; 9:11.
Wasikubali kuyumbishwa na vizuizi vyovyote 1 Wakorintho 6:12.
Wahakikishe wakati wote hawapandwi na hasira, 2 Timotheo 4:5.
Na wanaridhika kwa mambo yote, Wafilipi 4:11-12.

**Viongozi** wanatakiwa kujua maandiko, Yohana Mtakatifu 10:34; 19:28; Matendo ya Mitume: 20; 7:2-50; Warumi 10:16-21. Wanatakiwa kutunza utengamano Johana Mtakatifu 2:7; 3:10-12, 4:7, 11:14, na wanajua njia nzuri ya kuuliza maswali, Yohana Mtakatifu 7:14; 8:2; 1 Timotheo 4:11; Matendo ya Mitume 4:2; 5:21; 18:11; na pia kuandika, matendo ya Mitume 1:1; Romans 15:15; 2 Wakorintho 1:13.

**Viongozi na Kanisa**

**Viongozi** wanaouwezo wa kuunda maono ya siku za usoni, Yohana Mtakatifu 14:2, 14:12, ili kuwaandaa wanaowaongoza kuwa watumishi wa Mungu, Waefeso 4:12.

**Viongozi** Wanafanya kazi kwa kujituma, 1 Wakorintho 4:12,
Wanakuwa mfano hai kwa washirika wa kanisa, Yohana Mtakatifu 3:15,
Hawafanyi mambo kwa siri, Yohana Mtakatifu 18:20; Waefeso 6:21-22, na wanajizuia kufuata sheria na masharti yasio na msingi wowote, Yohana Mtakatifu 4:27; 5:18; 9:14.

**Viongozi** wanawapa nafasi ya utumishi watu wenye uwezo, Yohana Mtakatifu 4:1; Matendo ya Mitume 6:3, 2 Timotheo 2:2 na pia wanatambua washiriki nao wanahatarisha maisha sawia na wao, Yohana Mtakatifu 12:10; 17:14.
Wanawatuma wafuasi walio bora, Wafilipi 2:23, na kuwaleta watumishi wanyonge na wagonjwa katika sehemu salama, Wafilipi 2:25-30.

**Viongozi** wanatazama mambo kwa upana 1 Timotheo 5:21, wanapokabiliana na wenye fikra potovu, Wagalatia 2:11, inapobidi, wanahukumu watenda maovu, 1 Wakorintho 5:3, 12, au hata kuwahizima watenda dhambi wazi wazi  1 Timotheo 5:20.

**viongozi** wanatakiwa kusimamiwa kifedha na washiriki, 1 Wakorintho 9:1-12, ila wasiombe usimamizi huo wenyenye kwa washiriki 1 Wathesalonike 2:9; 2 Wathesalonike 3:8. 9:1-12.

**Viongozi** wawe na huruma na wajitoe kwa masikini, Warumi 15:26.
Waombee kanisa, 2 Wathesalonike 1:11
Wawe na moyo wa shukrani kwa watu wanaohudumia, 1 Wakorintho 1:4,
Wawachukulie waumini kama furaha na zawadi kutoka kwa Mungu, 1 Wathesalonike 2:19-20, Wakolosai 2:5.

**Viongozi** wajenge uhusiano wa kawaida na wanaume na wanawake wa rika zote 1 Timotheo 5:1-3.
**Kwa nini viongozi wanafanya wanayoyafanya**

**Viongozi** wanawapenda waumini, 1 Wathesalonike 2:8; Wafilipi 4:1, 1 Wakorintho 16:24; 2 Wakorintho 2:4, na wanao utawala wa huruma kama ule wa mzazi juu ya kanisa, Yohana Mtakatifu 13:33; 1 Wakorintho 4:15.

**Viongozi** wanawapa washiriki nafasi ya kuhudumu, Matendo ya Mitume 16:15, na wanawaomba kuwaombea, Waefeso 6:19; 2 Wathesalonike 3:1, Wakolosai 4:4.
Viongozi wanamaono, 2 Wakorintho 10:7; 4:18, na wao wenyewe wanafahamu wazi wazi hira za Shetani 2 Wakorintho 2:11.

**Viongozi** wanakubwa na mambo mengi 2 Wakorintho 1:5, magumu, vizuizi, kufungwa, kuvamiwa, wanakoswa usingizi, kukosa chakula na maji, wakati mwingi wako mbali na nyumbani, 1 Wakorintho 4:11; 2 Wakorintho 1:8; 6:4-5, 1 Wathesalonike 3:3-4, wakitambua kuwa yote ni kwa utukufu wa Mungu Wafilipi 1:13-14, 29; Warumi 18:23; 2 Wakorintho 5:2-4.

**Viongozi** wanashiriki katika mateso ya Kristo kwa wakati huu, na wanaamini watashiriki katika utukufu wake atakaporejea, Warumi 8:17; 1 Wakorintho 11:1; Waefeso 1:13.